# MIHOGO INAWEZA KUTUMIKA KUPUNGUZA GHARAMA YA JUU YA CHAKULA

29 Mei 2022



CHANZO CHA PICHA,GETTY IMAGES

Katika mfululizo wa barua zetu kutoka kwa waandishi wa habari wa Afrika, mwanahabari wa Ghana Elizabeth Ohene anazingatia wito wa Rais wa Uganda Yoweri Museveni kwa watu kula mihogo huku bei ya ngano ikipanda duniani kote.

Kuna mboga kuu mbili za mizizi katika Afrika Magharibi - mihogo na viazi vikuu au magimbi.

Muhogo unapatikana mwaka mzima, ni wa bei nafuu na unajulikana, au tukisema kwa usahihi, ulijulikana kuwa chakula cha maskini.

Nyingine maarufu ni viazi vikuu, ambayo mwandishi wa Nigeria Chinua Achebe alitaja kama "mfalme wa mazao".

Mavuno ya magimbi yanasubiriwa kwa hamu. Hakika, ibada maalum hufanywa kabla ya magimbi kuvunwa na kuliwa, na tunavaa nguo zetu bora zaidi ili kusherehekea zao hilo.

Muhogo ni chakula bora cha kila siku na kilikuwa kama chakula cha kawaida cha maskini na watumishi.

Ninaona kuwa Rais Yoweri Museveni wa Uganda anawataka watu wake kugeukia mlo wa mihogo kama dawa ya kuporomoka kwa bei ya ngano wakati huu ambapo gharama ya maisha duniani kote imepanda .

"Kama hakuna mkate, kuleni muwogo [mihogo]," alisema.



CHANZO CHA PICHA,GETTY IMAGES

Matamshi ya Bw Museveni yamezua utata, huku wakosoaji wakisema hana mpango wa kweli wa kukabiliana na gharama ya juu ya maisha.

Hapa Ghana, tulikuwa na waziri wa fedha ambaye, huko nyuma katika miaka ya 1960, alijaribu kuhalalisha pendekezo la ongezeko la kodi kwa kusema maskini hawataathirika kwa sababu walikula 'gari '- unga maarufu wa punjepunje uliotengenezwa kutokana na mihogo iliyochakatwa.

Wakati huo, 'gari' lilijulikana kwa kiasi kikubwa kama chakula cha maskini na waziri alisisitiza kwamba ukiongeza maji kwa nusu kikombe cha 'gari', itavimba na kutoa chakula cha kutosha kwa watu watatu. Ilikuwa ya bei nafuu .

Waziri pia alikuwa akitoa hoja, bila kusema kwa sauti, kwamba watu maskini hawakula mkate au wali, au vyakula vingine vya kifahari kutoka nje. Hii ilikuwa kweli kwa kiasi kikubwa wakati huo.

Miaka kadhaa baadaye, tulikuwa na waziri wa nchi ambaye alizungumzia kupanda kwa bei ya vyakula kwa kusema watu wanaweza kula kokonte, ambayo aliitaja kuwa mbadala wa bei nafuu kwa mchele na vyakula vingine kutoka nje.

Kokonte imetengenezwa kutoka kwa unga wa muhogo na, kama vitu vyote vya muhogo, ilijulikana kama chakula kinacholiwa na maskini.

Rais Museveni alitoa hoja kwamba alikula mihogo. Kwa maneno mengine, mtu yeyote asione aibu kula, au kuonekana anakula, mihogo kwa vile sasa ilikuwa chakula cha rais.

Siku hizi, zao hilo linalostahimili ukame pia linatajwa kuwa na faida za kiafya - mizizi ya muhogo haina gluteni, vitamini C nyingi na shaba nyingi.



CHANZO CHA PICHA,GETTY IMAGES

Maelezo ya picha,

Mizizi ya muhogo haina gluteni, vitamini C nyingi na shaba nyingi.

Sijui kama muhogo unabaki kuwa chakula cha maskini nchini Uganda, lakini Ghana tumetoka mbali.

Chukua gari. Inatoa taswira ya chakula cha wafanyikazi na maskini wakati ikawa mwandamani wa lazima wa wanafunzi wote wa shule ya bweni.

Wanaenda shuleni wakiwa na begi la 'gari' kwenye sanduku. Milo mbalimbali inayotengezwa na 'gari' kwenye mabweni huitwa 'kuloweka.'

Ni mchakato wa haraka na rahisi, hauhitaji kupika au tanuri ya microwave kwa ajili ya kupasha joto - unaweka 'gari'kwenye kikombe, kuongeza maji, sukari na maziwa, kuchanganya na hivyo tu. Una vitafunio vya kupendeza zaidi na vya kushibisha .

Mbadala ya kitamu ni maarufu zaidi na inahusisha kuchukua kikombe cha gari kavu, kunyunyiza maji kidogo juu yake ili kulainisha, kuongeza kijiko cha mchuzi wetu maarufu wa pilipili, shito, kuongeza bati la sardini, kuchanganya yote.Sijui kwanini lakini hii inaonekana bora kuliwa kwenye kikundi.

Lakini gari iligeuka kuwa bidhaa kuu ya vyakula vya asili wakati mhudumu maarufu wa Ghana, Barbara Baeta, alipobuni kichocheo cha "gari foto" - gari kilichochanganywa na changarawe na dagaa, ambacho alihudumia kwenye karamu ya serikali mwaka wa 1970 iliyoandaliwa na Waziri Mkuu Kofi Abrefa Busia. .

Ghafla gari kikawa chakula ambacho kilitolewa kwenye mikusanyiko ya watu wa juu na wenye nguvu na ilikuwa ya mtindo.

Kwa namna fulani, vyakula mbalimbali vinavyotengenezwa kwa muhogo vimegeuzwa kuwa vyakula ambavyo watu hujivunia kuvila.

Sio tofauti na kuibuka katika miaka ya 1960 kwa kile Waamerika wa Kiafrika walichokiita chakula cha roho, walipokumbatia kile walichokula kama watumwa na kugeuza kuwa vyakula vya mtindo na vinavyohitajika.

Nadhani kuna nafasi kwa baadhi ya wahudumu wa upishi wa Ghana kwenda Uganda na kuanzisha mikahawa ambayo inaweza kutoa vyakula vinavyotokana na muhogo pekee.

Na ninatumai kwamba wakati vita huko Ukraine utakapomalizika, mihogo itakuwa chakula bora katika Afrika na tutawaachia ngano wale wanaoikuza.

Kunaweza kusiwe na Chinua Achebe ambaye atazungumza kuhusu muhogo, huenda tusisherehekee sikukuu za muhogo lakini hakuna mtu atakayeitaja tena kama chakula cha maskini, na Rais Museveni hatalazimika kutoa hotuba ili kuwatia moyo watu wake kula mihogo.